



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA
BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI
TAARIFA KWA UMMA
USAJILI WA MITIHANI YA 28 YA PSPTB



Dodoma 19 Januari, 2024

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, mitihani ya 28 ya PSPTB inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **13/05/2024 mpaka tarehe 17/05/2024**. Watahiniwa wote wanaelekezwa kufanya usajili kwa kupitia <https://registration.psptb.go.tz> na pia kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **19/04/2024**. Mitihani hiyo itafanyika katika vituo vya ya **Dar es salaam, Moshi, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Zanzibar**.

WAOMBAJI WENYE SIFA KWA AJILI YA MITIHANI YA MEI, 2024

- (1) Wahitimu wote waliomaliza vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za shahada, stashahada na astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2023 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi.
- (2) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi katika sekta binafsi na umma bila kuwa na cheti cha CPSP.
- (3) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kwa ngazi za stashahada, shahada au sifa za kitaaluma kutoka Bodi ya taaluma husika.

NB. Watahiniwa wanaorudia mtihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana katika "bloc" moja kwa masomo kuanzia mawili hadi Sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani ya 28 ya PSPTB. Hivyo, wanashauriwa kuangalia ratiba ya mitihani kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia examinations@psptb.go.tz

GODFRED MBANYI
EXECUTIVE DIRECTOR